

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



Mtaa wa Sheikhbad,
S.L.P. 1004,
65101LINDI,
Barua Pepe: rbelindi@pccb.go.tz.
TANZANIA.

www.pccb.go.tz

LINDI – 26 .6. 2020

TAARIFA KWA UMMA

**TAKUKURU LINDI INAMSHIKILIA MTIA NIA PAMOJA NA
WAJUMBE WA HALMASHAURI KUU YA KATA - NAHUKAHUKA.**

NDG WANDISHI WAHABARI

Kupia kwenu, napenda kuujulisha umma kuwa TAKUKURU Mkoa wa Lindi inamshikilia mtia nia ambaye anatarajia kugombea ubunge katika jimbo la Mtama kupitia Chama Cha Mapinduzi na amekamatwa akiwa na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Kata ya Nahukahuka wapatao 23 Mtia nia kwa jina anaitwa MKULUNGWA ALLY CHINUMBA.

Mtia nia amekamatwa kufuatia taarifa zilizopokelewa na TAKUKURU mkoa wa Lindi zikieleza kuwa wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Kata ya NAHUKAHUKA wa Chama cha Mapinduzi wamekusanywa na mtia nia kwa lengo la kuwashawishi ili wampitishie kwenye kura za maoni kwani anatarajia kugombea nafasi ya Ubunge katika jimbo la Mtama katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Uchunguzi wa TAKUKURU mkoa wa Lindi umebaini kuwa mtia nia ni mzaliwa wa Kata ya Nahukahuka na ni Mhandisi katika Shirika la Ugavi wa Umeme - TANESCO MAKAO MAKUU , kwa maana hiyo ni mtumishi.

Mtia nia huyo alikamatwa akiwa na wajumbe nyumbani kwa ALLY CHINUMBA ambaye ni baba wa mtia nia.

Gari ya mtia nia lilipopekuliwa, kulikuwa na sh laki 841,000/= ambazo zilikuwa ndani ya gari lake lenye usajili namba T527 DEY ambazo ziliwekwa katika maeneo tofauti tofauti .

Ndani ya gari la mtia nia pia kulikuwa na bahasha ndogo dazani moja ambazo zinahisiwa ziliandaliwa kwa ajili ya kuweka fedha kwa ajili ya wajumbe.

TAKUKURU inaendelea na uchunguzi ili kubaini uvunjifu wa sheria.

TAKUKURU mkoa wa Lindi, kwa mara nyingine inaendelea kuwaonya wanaotarajia kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kuwa waache mara moja kujihusisha na vitendo vyovyote vinavyoashiria ni ushawishi kwa wapiga kura kabla, wakati na baada ya uchaguzi.

Wagombea wanaotarajia kugombea, wafuate utaratibu, kanuni na sheria. TAKUKURU tupo macho, wala hatutafumbia vitendo vyovyote vinavyolenga kumshawishi mpiga kura kwa namna yoyote ile. Hiki siyo kipindi cha kuijaribu TAKUKURU. Mgombea yeyote anayejihushisha na vitendo vilivyokatazwa, hatutamwonea aibu, atakamtwa na hatua zitachukuliwa.

Imetolewa na:

Charles Mulebya

NAIBU Mkuu wa TAKUKURU (M) Lindi